# JARIBIO LA MTIHANI

## DARASA LA TANO - MWAKA 2021

STEP FLYER SERIES — STEP FLYER — 007

# KISWAHILI:LUGHA

5

**SEHEMU YA KWANZA:LUGHA** *Muda: Saa 1 Dakika 40*

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.
2. Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-
   *(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako*

---

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne.***

***Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa..***

Shalom ni msichana ____1____ shule ____2____. Ana adabu ____3____ na tabia ____4____ na kila mtu anampenda. Zaidi ya hayo,Shalom ni msichana ____5____kuliko wote shuleni. Anaoga kila siku____6____ maji safi. Nywele____7____ni fupi si____8____. Huzichana vizuri akitumia kitana. Anapenda masomo____9____yanayofundishwa shuleni. ____10____ sote tunamfurahia shalom. ____11____ anajua kuwa uchafu ni kitu____12____. Anatupa uchafu____13____ mbali na nyumba____14____. Shalom ni msichana____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A.kwa | B.ya | C.wa | D.cha |
| **2.** | A.letu | B.wetu | C.kwetu | D.yetu |
| **3.** | A.zuri | B.nzuri | C.mzuri | D.kizuri |
| **4.** | A.njema | B.jema | C.mwema | D.chema |
| **5.** | A.msafi | B.chafu | C.safi | D.kichafu |
| **6.** | A.na | B.kwa | C.ya | D.wa |
| **7.** | A.zake | B.yake | C.wake | D.vyake |
| **8.** | A.refu | B.ndefu | C.ndevu | D.mrefu |
| **9.** | A.wote | B.zote | C.yote | D.vyote |
| **10.** | A.Nyinyi | B.Wao | C.Wewe | D.Sisi |
| **11.** | A.Yeye | B.Mimi | C.Nao | D.Nayo |
| **12.** | A.mbaya | B.kibaya | C.baya | D.vibaya |
| **13.** | A.wowote | B.yeyote | C.chochote | D.lolote |
| **14.** | A.wao | B.yetu | C.mwao | D.yao |
| **15.** | A.chema | B.mwema | C.kwema | D.njema |

***<u>Kutoka swali la 16 hadi 30; jibu kulingana na maagizo.</u>***

16. Akisami $^{3}/_{4}$ huitwa

A. robo tatu
B. thuluthi nne
C. tatu na nne
D. tatu kwa nne

17. Kinda ni kwa ndege kama vile ________ ni kwa chura.

A. kimatu
B. kisui
C. kiluwiluwi
D. kinyemere

18. Tumia kiulizi **'pi'** kwa usahihi:

Ua ________unabomolewa na mafundi?

A. lipi
B. zipi
C. ngapi
D. upi


19. Mmea uzaao kahawa huitwa

A. kahawa
B. mbuni
C. fenesi
D. mgomba

20. Mamaye mzazi wako wa kike utamwitaje?

A. Mavyaa
B. Halati
C. Nyanya
D. Wifi

21. Umbo hili huitwa



A. pia
B. mraba
C. mche mraba
D. mche mstatili

22. Nomino **"gari"** liko katika ngeli ipi?

A. LI-YA
B. I - ZI
C. A - WA
D. U - ZI

23. Eleza maana ya sentensi hii

**Mkoba huu ni nanga**

A. Mwepesi
B. Mzito
C. Mpya
D. Mzee

24. Maamkizi **'alamsiki'** hutumika wakati gani?

A. Asubuhi
B. Mchana
C. Alfajiri
D. Jioni

25. Ni sentensi ipi isiyoakifishwa vizuri?

A. Umefanya kazi ya ziada?
B. Kwa kweli, yeye anafanya juhudi.
C. Mjakazi alinunua, muwa, ndimu, chumvi, na sukari
D. Lo! Bao la kwanza.

26. Tegua kitendawili kifuatacho

**Ndugu ambaye ukikutana naye watu hulia.**

A. Harusi
B. Meno
C. Nyayo
D. Kifo

27. Andika sentensi hii kwa wingi:

**Karatasi imeraruka**

A. Makaratasi zimeraruka
B. Karatasi imeraruka
C. Makaratasi zimeraruka
D. Makaratasi yameraruka

28. **Jaza pengo kwa neno sahihi.**

Ukimwi________ugonjwa unaoua watu wengi.

A. ndio
B. ndiyo
C. ndizo
D. ndimi

29. Ni ipi si sehemu ya ndani ya mwili?

A. Kitovu
B. Kibofu
C. Nyongo
D. Figo

30. **Jaza pengo kwa jibu sahihi**

________kula viazi vitamu kuliko chipsi.

A. Ni bure
B. Ni heri
C. Ni hasira
D. Ni ngumu

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 -40.***

Sote tuliamka bukrata wa shiya na kujihami kwa sime, mshale kwenye podo na uta pamoja na ngao. Tulikusanyika kwenye njia panda kilomita tano kutoka kijijini mwetu.

Nyuso zetu zilikunjana, ishara ya ushupavu tuliokuwa nao katika kazi hiyo ya usasi. Jua lilikuwa likichoma kwa miale ya njano kwani ulikuwa ni msimu wa kiangazi.

Msitu ule ulionekana mkuu lakini nikapiga moyo konde. Tulijitoma mle ndani tukiwa tumeuzingira. Sote tulipiga kamsa kuwaondoa kwa kishindo nyati wale ambao jana yake walikuwa wamevamia bustani moja la chifu wa kata yetu.

Mara tukasikia kijibwa chetu kimoja kimepiga kamsa ambazo zilifanya malaika yetu kutusimama tisti. Pumzi zilituisha na tukawa katika hali ya taharuki. Ikawa ni vuta nikuvute. Hatujui twende mbele au nyuma.

Ghafka bin buu, nyati wale ambao walikuwa wamelala kifudifudi walitugeukia kuwa pepo wabaya. Pale tuliamua mguu niponye kila mmoja akielekea upande wake,tulitawanyika huku tukiwacha silaha zote zile kichakani.

---

**31.** Kwa nini watu hawa waliamua kwenda kuwasaka wanyama wale?
A. Walitaka mto wa nyama
B. Walikuwa wakifanya mazoezi
C. Walipenda usasi
D. Wanyama hao walivamia bustani la chifu

**32.** Njia panda ni
A. njia mbili
B. njia zinapogawanyika
C. mahali pasipo na njia
D. njia iliyopanda

**33.** Watu waliokuwa wanaenda kuwasaka wanyama walikusanyika umbali gani kutoka kijijini mwao?
A. Mita tano
B. Kilomita tano
C. Mita mia tano
D. Maili tano

**34.** Taja jina moja la vitu vifuatavyo; sime, mshale, podo, uta
A. Ala za muziki
B. Zana za vita
C. Zana za usafiri
D. Ala za vita

**35.** Wasasi walikuwa wameenda kuwinda msimu gani?
A. Masika
B. Vuli
C. Kiangazi
D. Kipupwe

**36.** Kupiga kamsa ni
A. kuzungumza kwa sauti
B. kucheka kwa sauti
C. kurusha mawe ili kuwafurusha wanyama
D. kupiga mayowe

**37.** ***"Malaika yetu kutusimama tisti"*** Malaika ni nini kulingana na taarifa hii?
A. Viumbe wa Mungu wenye nguvu nyingi
B. Mtoto mchanga
C. Nywele zinazomea juu ya mwili
D. Nywele zinazomea kwenye sehemu ya masikio

**38.** Mwandishi anasema nyati walilala kifudifudi kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari ni
A. kulala ovyo ovyo
B. kulala chali
C. kulala na kukoroma
D. kulala tumbo likiwa chini

**39.** Ni kweli kusema kuwa
A. wawindaji walitishika wakawacha silaha zao
B. wawindaji waliwauwa nyati
C. wawindaji hawakuingia msituni
D. wawindaji hawakubeba ngao

**40.** Ukubwa wa nomino **'kijibwa'** kwa mujibu wa taarifa ni:
A. mbwa
B. jibwa
C. lijibwa
D. jimbwa

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali kutoka 41-50.***

Jina langu ni Kiprono. Wanafunzi wenzangu wananiita Kip. Hilo si jina langu. Hilo ni jina la utani tu. Sikilizeni nitawaambia kwa nini ninaitwa jina la Kip. Jina la kubandikwa.

Wakati shule zinapofungwa,sisi humzuru nyanya yetu. Nyanya yetu huishi Kapsabet. Yeye ana bustani kubwa sana. Katika bustani hilo yeye hufuga ng'ombe, kuku, bata na bata mzinga.

Nilienda kumtembelea nyanya yangu likizo moja. Nilipokuwa huko, nilimwonyesha jino langu. Lilikuwa linaregarega. Lilitaka kung'oka.

Nyanya aliliangalia jino hilo kwa makini na kuniambia ni lazima ling'olewe. Mimi sikutaka jino langu ling'olewe lakini nyanya yangu alinibembeleza. Nyanya alinionya kwamba nisingeling'oa meno yangu yangepandana. Nilitafakari taswira ya maneno yake nyanya nikaona kwamba,ningekuwa kama fuko.

Basi niling'olewa jino hilo na damu ikanitoka. Nilianza kuogopa nilipoona damu. Niliingia chumbani mwangu nikajitazama. Lo! Eh! Nilikuwa na pengo kubwa sana. Nyanya aliona hofu yangu lakini akanipa moyo.

Niliporudi shuleni wanafunzi walinicheka na kuniimbia hivi; Kip kipengo Kipe, ukimtazama kweli utacheka. Jina la utani nikapata hapo.

---

**41.** Tunaweza kusema **"kip"** ni jina

A. halisi B. la ukoo
C. jazi D. geni

**42.** Ni nini maana ya neno **'humzuru'** kulingana na taarifa?

A. humtembelea B. hupotea
C. humsalimia D. humpelekea

**43.** Nyanya wa mwandishi wa habari hii anaishi wapi?

A. Narok B. Kapenguria
C. Kapsabet D. Kabarnet

**44.** Kati ya wanyama hawa, ni yupi hajatajwa kwenye habari hii?

A. Ng'ombe
B. Bata mzinga
C. Kuku
D. Punda

**45.** Kiprono alikuwa ameenda kumzuru nyanya yake wakati gani?

A. Wakati wa shule
B. Siku ya Jumapili
C. Wakati wa likizo
D. Wakati wa sherehe

**46.** Kwa nini mwandishi alianza kuogopa?

A. Jino lake liling'oka kwa kishindo
B. Alidhani angeng'olewa jino angeaga dunia
C. Nyanya yake alimtisha sana
D. Aliona damu jino lilipong'olewa

**47.** **'Lo! Eh!'** ni maneno yaliyotumiwa katika taarifa. Yanatoa maana ya

A. kuuliza swali
B. kushangaa
C. kutafakari
D. kubabaika

**48.** Nyanya aliona hofu lakini **akanipa moyo**. Usemi uliopigiwa mstari maana yake ni;

A. kuhimiza mtu avumilie
B. kuogopa sana
C. kutia hofu
D. kustaajabu sana

**49.** Nyanya alimpa Kiprono sababu gani ya kuling'oa jino lililoregarega?

A. Asipoling'oa angekuwa kama fuko
B. Asipoling'oa hangependwa na wanafunzi wenzake
C. Asipoling'oa meno yake yangepandana
D. Asipoling'oa hangeenda shuleni tena.

**50.** Kwa nini wanafunzi walimcheka mwandishi?

A. Alikuwa na pengo kubwa
B. Alikuwa na meno yaliyopandana
C. Alikuwa kibogoyo
D. Alipendeza sana kwao